


Tusi watupiliye wahanga wa ubakaji!


Tuwaunge mkono kadiri tunaweza!




Un message du Bureau Conjoint des Nations Unies aux Droits de l'Homme et du Bureau de l'Information Publique de la MONUSCO

ALIBAKWA.

Una waza kama uta ishi vizuri bila yeye?
Na yeye, namna gani ata ishi bila wewe?



Jirani yako, rafiki yako



Bibi yako mama yako



Mchumba wako, rafiki yako

Kumubaka ni kumuwa muhanga kimwili na kimafikiri.

Kuachiliwa na bwana, na jamaa, na jamii kwa sababu ulibakwa ni kumuwa mara mbili muhanga.

Kama muhanga ananyamanza kwa kuwa ana woga ao anasikiya haya:

- **Haendi kwa kipimo ya mganga hapo hapo baada kitendo cha ubakaji** na kusababisha vinyume vingi sana kwa afya na kwa maisha ya muhanga.
- **Hatafute kupokeya huduma wa kimafikiri:** ubakaji ni hali inayo tesa kwa kiasi ambayo wahanga hawawezi shinda hali wenyewe.
- **Hastaki mubakaji kwenyi korti.** Ile inaongezea wabakaji kiburi na kuhatarisha wengine wamama, wabinti na watoto.
- **Ana pinga kwa kufaidishwa na kazi za kumurudisha katika hali ya kijamii na kiuchumi.** Kama ana nyamanza hata faidishwa na zile kazi ambazo zinaweza kuwa msaada mkubwa kwa jamaa lake pia.

Wahanga wa ubakaji hawana kamwe daraka kwa hali iliyo wafikia. Mubakaji anapashwa azibiwa hapana wahanga.

Muhanga wa ubakaji anapashwa tiliwa moyo kwa:

- **Kwenda kwenyi hospitali munamo masaa 72 ama mbele ya siku tatu** kwa kuepuka uambukizo wa ukimwi, ambukizo zakupitiya kwenye viungo vya uzazi na kupata kitambulisho cha mganga kitakacho musaidiya kuhakikisha kitendo cha ubakaji nafasi mbalimbali sawa vile korti.
- **Kukutana na nyumba ya usikilizi** na ya usindikizaji ambazo zita weza msaidiya kwa kushinda majehuri yote alizo zipata.
- **Kumtowa na kumstaki mubakaji kwenye korti.** Ana weza hudumiwa kwa bure na shirika fulani na kupata azabu ya yule mbakaji na kurudishiya muhanga haki zake.
- **Kutanana na kituo cha kumurudisha katika hali ya kijamii mahali** anaweza faidishwa na msaada kwa kufundishwa kazi za mikono ao kuanza kazi, ya uchuuzi akitumia pesa alizozipewa kama mpoko.